**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA WAZIRI MKUU-TAMISEMI**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**

# MANEROMANGO SEKONDARI

**SIMU NA.**
**Mkuu wa shule – 0713373594**
**Makamu M/Shule – 0682064821**
**Patron- 0675063882**
**Matron-0697063614**
EMAIL: maneromangosec@gmail.com
S.L.P 28085

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ……………………………………………………**
**S.L.P ……………………………**
**……………………………**

**YAH: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE MKOA WA PWANI**

1. Nafurahi kukujulisha kuwa, umechaguliwa kujiunga na shule hii kidato cha tano mwaka …………… na atasoma tahasusi ya ………. Napenda kuchukuwa nafasi hii kukupongeza na kukukaribisha hapa shuleni na bila shaka utapenda kuishi na kunufaika na mambo yanayoendeshwa hapa shuleni. Nategemea kwamba muda wote utakapokuwa katika shule hii utashirikiana na wanafunzi wenzako, walimu na wafanyakazi wasio walimu katika kutoa mchango wako wa mawazo na vitendo ili kuleta na kudumisha sifa nzuri na maendeleo ya shule hii.

   Shule ya Sekondari Maneromango ipo katika Wilaya ya Kisarawe, Mkoa wa Pwani, umbali wa kilometa 65 kutoka Dar es salaam. Unapokuja Maneromango itabidi upande mabasi yanayokwenda Msanga au Maneromango. Mabasi yanaanzia safari katika kituo cha Pugu –kigogo sokoni jijini Dar es Salaam nauli shilingi 7,000/= Pamoja na barua hii naambatanisha taarifa zifuatazo:

   **(a)** Fomu ya kujiunga na shule (Joining Instructions) – hakikisha unaisoma neno kwa neno.

   **(b)** Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi (MSS.K5. A) na Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule (MSS.K5. B). Fomu hizi zitatakiwa kujazwa na mzazi/mlezi na utazileta shuleni na kuzikabidhi siku ya kuripoti.

   **(c)** Fomu ya uchunguzi wa afya (MSS.K5).

Mwisho, nakufahamisha kuwa muhula wa masomo unaanza tarehe ………….. hivyo,unatakiwa **ufike shuleni** kuanzia tarehe …………… na mwisho ni tarehe ……….. Fika **kabla ya saa kumi na mbili (12:00) jioni**. Mara ufikapo shuleni utapokelewa na mwalimu wa zamu ambaye atakupeleka ofisi ya malezi ambapo utasajiliwa. Kama utachelewa kuripoti nitaiarifu Wizara (TAMISEMI) ili waweze kuchagua mwanafunzi mwingine wa kuchukua nafasi yako. Nakutakia safari njema.

Karibu Maneromango.

……………………..
**PILI MWAJIRI**
**MKUU WA SHULE**
**SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO**

**FOMU YA MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (JOINING INSTRUCTIONS)**

**Soma maelezo haya kwa uangalifu na umakini na uyatekeleze**;

## 2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA: -

### 2.1 SARE ZA SHULE

Unatakiwa uje na sare ya shule kama ifuatavyo na **uwe na idadi ya kutosha** ;

i. Sare ya shule hii ni sketi 2 **NDEFU HADI CHINI** kwa wasichana mshono wa **rindaboxi** na Suruali 2 kwa wavulana **NDEFU ZISIZOBANA** zenye **MARINDA MAWILI** na **Pindo ya nje (turn up)**, rangi bluu nyeusi (**Dark blue**).

ii. Mashati 2 meupe ya mikono mirefu

iii. Kwa wanafunzi wa kiislamu waje na hijabu (kijuba) nyeupe 2 ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama zisizo na urembo wala maua (plain). (Jalabibi haziruhusiwi)

iv. Sare ya michezo jezi ya timu ya taifa stars rangi ya bluu iliyoandikwa **TANZANIA** kwa mbele (T-shirt na bukta)

v. Viatu vyeusi vya kufunga na Kamba na vyenye visigino vifupi. vi. Soksi jozi 2 nyeusi kwa wavulana na nyeupe kwa wasichana. vii. Mkanda mweusi wa ngozi wa kuvalia suruali kwa wavulana.

viii. Sweta la shule rangi ya suruali/sketi (Dark bluu) lenye muundo wa "V"mbele.

ix. Nguo za kushindia(shamba dress)Sketi nyeusi **NDEFU HADI CHINI** kwa wasichana mshono wa **rindaboxi** na T-shirt nyekundu yenye nembo ya shule, suruali nyeusi **ndefu zisizobana** zenye **marinda mawili na pindo ya nje (turn up)** kwa wavulana na T-shirt ya kijani yenye nembo ya shule kwa ajili ya kushindia, (T-shirt zote form six zenye nembo ya shule zinapatikana duka karibu na shule)

x. T-shirt ya shule rangi ya bluu yenye nembo ya shule (zinapatikana duka karibu na shule)

xi. Traki suti dark blue zisizobana na isiyo na maandishi wala picha mbele na nyuma.

xii. Raba za michezo jozi 1. (rangi yoyote)

**NB**: **Zingatia rangi na maelekezo yote ya sare za shule, nguo za nyumbani haziruhusiwi**

### 2.2 MAHITAJI MENGINE MUHIMU AMBAYO MWANAFUNZI ANAPASWA KUJA NAYO SHULENI: -

i Madaftari makubwa (Counter Books-Quire 3 au Quire4)

ii Photocopy paper (Ream A4 size) aina ya DOUBLE A, MAESTRO STANDARD, TOP KOPIE, ulete ream moja kwa kila mwaka na Ruled paper (karatasi za mistari) ulete moja kwa kila mwaka.

iii Scientific calculator (kwa masomo ya science na hisabati).

iv Godoro lenye upana wa futi 2.5

v Mashuka jozi 2 (rangi ya bluu bahari kwa wavulana na rangi ya pinki kwa wasichana), blanketi 1, foronya ya godoro 1, taulo na chandarua 1 rangi nyeupe na Nguo za ndani za kutosha

vi Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kikombe na kijiko)

vii Sanduku la bati na kufuli lake kwa usalama wa vifaa vyake Laboratory coat, stop watch, na 'thermometer' (kwa Physics na Chemistry).

viii Ndoo 2 ndogo(lita kumi) zenye mifuniko

ix (a). Fyekeo 1 (Kwanja), Soft bloom 1 (fagio refu laini la ndani) kwa PCM
(b). Jembe lenye mpini 1 na Squizer (rubber squeezer) kwa HKL.
(c). Panga 1 na fagio gumu (Hard bloom) 1 kwa HGFa
(d) Fyekeo 1 na Brashi ngumu ya kusugulia chooni. (Toilet brush) HGLi

**x. Mwanafunzi lazima aje na cheti cha kuzaliwa na result slip. (Halisi na kivuli (copy).**

2.3 **MICHANGO MBALIMBALI**

| Na. | AINA YA MCHANGO | KIDATO CHA TANO | KIDATO CHA SITA |
|---|---|---|---|
| 1. | Michango ya uendeshaji wa shule | 65,000 | 65,000 |
| 2. | Kitambulisho cha shule | 5,000 | - |
| 3. | Tahadhari (caution money) | 5,000 | 5,000 |
| 4. | Nembo ya shule | 5,000 | - |
| | **JUMLA** | 8**0,000** | 7**0,000** |

**Zingatia:**

- Fedha hizo zilipwe kwenye Akaunti ya shule Namba: **21401100004**, Jina la Akaunti ni **MANEROMANGO SECONDARY SCHOOL**, benki ya NMB.
- **Hakikisha unaandika jina la mwanafunzi kwenye pay-in-slip**
- Nakala ya 'slip' ya benki utakayolipia ilete shuleni, hakikisha umeiandika kwa nyuma mchanganuo wa fedha uliyoilipa kwa kila mchango.
- **Tarehe ………… kutakuwa na kikao cha wazazi na Bodi ya shule kitaambatana na visiting day kwa Mwezi huo.**

## 3. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sharia ya Elimu namba 10 ya mwaka 1995. Aidha ,inazingatia miongozo yote inayyotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu- TAMISEMI Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na kanuni za shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa jumla ni jambo la lazima.
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule.
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku (preparation).
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule atakazo pewa.
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
v. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule.
vi. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
vii. Kutunza mali za shule.
viii. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari, na mwalimu wa afya

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi.**
- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika kwa mwanafunzi mmoja tu.**
- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalumu toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa)**
- **Kila mwanafunzi anapaswa kuja na BIMA YA AFYA, kwa asiyekuwa na Bima aje na TSH: 50,400/= Ili aweze kukatiwa Bima ya Afya.**

**MZAZI AU MLEZI HURUHUSIWI KUMWONA MWANAFUNZI SHULENI BILA RUHUSA KUTOKA UTAWALA:**
**Siku za kuwaona (visiting day) wanafunzi ni kila ijumaa ya mwisho wa mwezi muda wa kazi ili uweze kujua maendeleo ya mwanao kitaaluma**

**3.2 Makosa yatakayosababisha mwanafunzi kufukuzwa shule ni pamoja na;**

i. Wizi
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo.
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au na mtu yeyote yule.
vi. Kusuka nywele kwa mtindo usiokubalika.Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni
vii. Kufuga ndevu
viii. Ulevi au unywaji pombe na matumizi ya dawa za kulevya na sigara
x. Uasherati, uhusiano wa jinsi moja, kuoa au kuolewa.
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba.
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi
xiii. Kusababisha mimba au kumpa mimba msichana
xiv. Kutembelea majumba ya starehe ,nyumba za kulala wageni na vibanda vya kuangalia mipira.
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi isiyo rasimi katika mazingira ya shule.
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k
xviii. Uharibifu wa mali ya Umma kwa makusudi

**ANGALIZO:** Mwanafunzi wa kike hawaruhusiwi kusuka nywele.

**4. Viambatanisho na fomu Muhimu**

- Fomu ya Uchunguzi wa afya (Medical Examination form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa hospitali ya Serikali,
- Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi / mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai,
- Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule, na
- Picha nne (2) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafuzni wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na namba za simu

**5.** Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgonjwa na yuko mahututi hivyo mazazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO**
**USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA**
**ZIFUATAZO:** -

- **Mkuu wa shule – 0713373594**
- **Makamu M/Shule – 0682064821**
- **Mwandamizi Taaluma -0678481652**
- **Patron- 0675063882**
- **Matron-0697063614**

## MISHONO NA RANGI YA SARE ZA SHULE







**ORODHA YA VITABU VYA MASOMO (mzazi unaweza ukamnunulia mwanao)**

**SOMO LA PHYSICS (PCM)**

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| **PHYSICS** | | | |
| Advanced Level Physics (7th edition) | Nelkon and Parker | Heinemann | 1995 |
| S. Chand’s Principles of Physics (Class XI) | V.K. Mehta & Rohit Mehta | S. Chand Publishing | N/A |
| Physics for Advanced Level - Form Five | TIE | Tanzania Institute of Ed. | N/A |
| **CHEMISTRY (PCM)** | | | |
| Physical Chemistry (New edition) | Ngaiza | N/A | N/A |
| General and Inorganic Chemistry | TIE | Tanzania Institute of Ed. | N/A |
| Physical Chemistry (4th edition) | Raymond Chang | McGraw-Hill | N/A |
| **GEOGRAPHY(HGFa&HGLi)** | | | |
| Principles of Physical Geography | F.J. Monkhouse | Hodder Education | N/A |
| Geography: An Integrated Approach | David Waugh | Nelson Thornes | N/A |
| **MATHEMATICS (PCM)** | | | |
| Advanced Mathematics Book 1 and 2 | J.K. Backhouse | Longman | N/A |
| Conceptual Mathematics Form Five | Mayombya | N/A | N/A |

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| **HISTORY(HKL,HGLi&HGFa)** | | | |
| History for Advanced Secondary Schools | TIE | Tanzania Institute of Ed. | 2024 |
| The Ultimate Principles of History One | B. Magoti | N/A | 2025 |

**SOMO LA ENGLISH LANGUAGE (HKL)**

## NOVEL

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Animal Farm | George Orwell | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| Chasing the Leopard Finding the Lion | Julie Wakeman-Linn | Mkuki na Nyota Publishers Ltd | 2024 |
| The Opportunist | Nyambari C. M. | Mbesa Books Distributors | 2023 |
| The Horizon Unveiled | Elite Nyangwine Fellowes Mwaisela | FGD Tanzania Ltd | 2011 |

## PLAY

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| The Government Inspector | Nikolai V. Gogol | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| An Enemy of the People | Henrik Ibsen | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| A Taste of Heaven | Farouk Topan | Mkuki na Nyota Publishers Ltd | 2023 |

## POETRY

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Summons: Poems From Tanzania | Richard S. Mabala et al. | Mkuki na Nyota Publishers | 2023 |
| Lament of the Silent & Other Poems | Jared Angira | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |

**FASIHI YA KISWAHILI(HGFa)**

## RIWAYA

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Vuta N'kuvute | Shafi Adam Shafi | Mkuki na Nyota Publishers Ltd | 2007 |
| Asali Chungu | Said Ahmed Mohamed | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| Mwana wa Yungi Hulewa | Mohammed Said Abdulla | East African Educational Publishers Ltd | 2023 |
| Vipuli vya Figo | Emmanuel Mbogo | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |

## TAMTHILIYA

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Kaptula la Marx | Euphrase Kezilahabi | Africa Proper Education Network | 2023 |
| Nyerere na Safari ya Kanaani | Emmanuel Mbogo | Africa Proper Education Network | 2023 |
| Morani | Emmanuel Mbogo | Africa Proper Education | 2007 |

| | | Network | |
|---|---|---|---|

## USHAIRI

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Dhifa | Euphrase Kezilahabi | Africa Proper Education Network | 2023 |
| Utenzi Majumui wa Karne ya 21 | Idd M. Nyambari Nyangwine | Mwimbe Publishers | 2023 |
| Malenga wa Bara | M.M Mulokozi na K.K Kahigi | African Proper Education Network | 2023 |
| Fungate ya Uhuru | Mohamed Seif Khatibu | Africa Proper Education Network | 2007 |

# SOMO LA KISWAHILI(HKL)

## RIWAYA

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Dunia Uwanja wa Fujo | Euphrase Kezilahabi | Africa Proper Education Network | 2023 |
| Ua la Faraja | W.E. Mkufya | Mangrove Publishers | 2007 |
| Mirathi ya Hatari | C. G. Mung'ong'o | Mkuki na Nyota Publishers Ltd | 2023 |
| Wasifu wa Siti Binti Saad | Shaaban Robert | Mkuki na Nyota Publishers Ltd | 2023 |

## TAMTHILIYA

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Mukwava wa Uhehe | M. M. Mulokozi | Africa Proper Education Network | 2023 |
| Shujaa Mirambo | Emmanuel Mbogo | Africa Proper Education Network | 2023 |
| Usaliti Mjini | Francis Imbuga | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |

## USHAIRI

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Fumbo Linaloelea | Nyambari C. M. Nyangwine | Mbesa Books Distributors | 2023 |
| Malenga wa Ziwa Kuu | Wallah Bin Wallah | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| Andamo, Msafiri Safarini | Ghassani Mohammed Khelef | Educational Books Publishers Ltd | 2023 |
| Wosia wa Baba | Amanzy Ahmed Mohamed | Abantu Publications Ltd | 2024 |

# SOMO LA LITERATURE IN ENGLISH(HGLi)

## NOVEL

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Arrow of God | Chinua Achebe | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| A Man of the People | Chinua Achebe | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| A Grain of Wheat | Ngugi wa Thiong'o | East African Educational Publishers Ltd | 2023 |
| Petals of Blood | Ngugi wa Thiong'o | East African Educational Publishers Ltd | 2023 |
| No Longer at Ease | Chinua Achebe | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| Joy Comes in the Morning | Hopolang Phororo | Mkuki na Nyota Publishers Ltd | 2023 |
| The Lion of Yola | Severine Ndunguru | E& D Vision Publishing | 2010 |

## PLAY

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Betrayal in the City | Francis Imbuga | East African Educational Publishers Ltd | 2023 |
| I Will Marry When I Want | Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mirii | East African Educational Publishers Ltd | 2023 |
| Julius Caesar | William Shakespeare | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| Man of Kafira | Francis Imbuga | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |

## POETRY

| TITLE | AUTHOR | PUBLISHER | YEAR |
|---|---|---|---|
| Boundless Voices Poem From Kenya | Arthur I. Luvai | East African Educational Publishers Ltd | 2024 |
| The Bleeding Heart and Other Poems | Shilia Kaaya | FGD Tanzania Ltd | 2009 |

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**
SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO
**FOMU YA MAELEZO BINAFSI KUHUSU HISTORIA YA MWANAFUNZI**

**MSS.K5. A**

**1.** Jina lako kamili…………………………………………………

**2.** Kidato ulichojiunga hapa shuleni……………………..mchepuo…………………

**3.** Jina la mzazi/mlezi…………………………………………..
Anuani yake…………………………Simu ya Ofisini…………………………..simu ya mkononi……………………………… Kazi yake…………………………………………..

**4.** Mahali ulipozaliwa
(i) Mkoa……………………… Wilaya ………………… Kata……………
(ii) Tarafa……………………… Kijiji cha …………………………..
(iii) Tarehe ya kuzaliwa ……………………..

**5.** Mahali unapoishi sasa……………………………………… Anuani yako…………………………..
Namba za simu……………………………

**6.** Dini/dhehebu lako……………………..

**7.** Unaishi na Baba tu/mama tu/wazazi wote/mlezi…………………………..

**8**. Shule ya sekondari uliyomalizia………………………Anuani…………………..

**9.** Michezo unayocheza
(a)…………………………………
(b) …………………………………

**10.** Vyama vya kujifunza ambavyo wewe unapenda kuwa mwanachama: Scout, Fema, Wapinga Rushwa(PPCB), YUNA, Mali Hai,Ant Aids, School Magazine na Mazingira.
(a)…………………………………………..
(b)……………………………………………
(c)……………………………………………

**11.** Je unao ulemavu wowote? (Ndiyo / Hapana)
Kama Ndiyo taja aina ya ulemavu…………………………………………………..

**12. MKATABA WA KUTOSHIRIKI KATIKA MIGOMO, FUJO NA MAKOSA YA JINAI**

Mimi ………………………………………niliyechaguliwa kujiunga na kidato cha tano (V) katika shule ya sekondari ya Maneromango, nimesoma kwa makini sheria na taratibu za shule nikiwa na wazazi/walezi wangu.Nimejadiliana nao na nimezielewa vema kabisa. Naahidi/nathibitisha kuwa sitashiriki migomo au kuhamasisha mgomo, fujo na sitofanya makosa ya jinai.

Saini ya mwanafunzi: ………………….. tarehe …………………………..

HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE

**SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO**

## FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO

## MENGINE YANAYOTOLEWA NA SHULE

MSS.K5. B

Fomu hii ijazwe na mzazi au Mlezi wa mwanafunzi katika sehemu zake na irudishwe shuleni ikiwa imeambatanishwa na picha ya mzazi/mlezi. Shule itatoa taarifa kwa mzazi / mlezi ambaye picha yake na maelezo yake yataonekana katika fomu hii.

Mimi……………………………………………mzazi/mlezi wa mtoto wangu ……………………………………nimeona, nimeelewa na nimekubali masharti yote yanayohusu mtoto wangu kujiunga na shule ya sekondari ya Maneromango.

Nitampa mahitaji yote yanayotakiwa na nitashirikiana na walimu wa shule ya Maneromango katika kumlea vizuri mtoto wangu ili aweze kusoma na kuelewa na hatimaye aweze kufanya mitihani yote ya ndani shuleni na ya Taifa kwa mujibu wa ratiba.

Saini ya mzazi/mlezi…………………

Anuani ya mzazi/mlezi

………………………..

…………………………..

Simu………………………..

**TAMKO LA MZAZI/MLEZI:**

Mimi…………………………………………… mzazi/mlezi wa

mwanafunzi………………………………………………wa kidato cha tano.

Nakiri kwamba yaliyoandikwa hapo juu kwenye fomu zote mbili (MSS.K5. A na MSS.K5.B) ni sahihi.

| | |
|---|---|
| Picha ya mwanafunzi | Picha ya mzazi/mlezi |

**SAINI YA MZAZI/MLEZI**

…………………………………..

Tarehe…………………………..

**Ndugu/jamaa/marafiki wa karibu na muhimu wanaoweza kuwa msaada kwa mwanafunzi**

Wafuatao ni ndugu/rafiki zangu wa karibu ambao wanaweza kunisaidia kama kuna dharura.(Ni vema wakawa watu wazima )

| Na. | Jina la ndugu/rafiki | Anwani ya anapopatikana | Simu(INAYOPATIKANA) | Uhusiano |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | | | | |
| **2.** | | | | |
| **3.** | | | | |

Picha za ndugu/jamaa/rafiki walioandikwa hapo juu

Bandika picha (Passport size) ya ndugu/jamaa

JINA. ……………………
Simu……………………

Bandika picha (Passport size) ya ndugu/jamaa

JINA……………………
Simu……………………

**HALMASHAURI YA WILAYA YA KISARAWE**

**SHULE YA SEKONDARI MANEROMANGO**

**FOMU YA UCHUNGUZI WA AFYA MSS.K5.**

(Request for Medical Examination)

This form is to be completed by a Medical Officer.

**Name of Student:** ………………………………………… **Age:** ……. **Sex:** …………

The above named has been examined in respect of:

**(a) STOOL** ………………………………………………………………………….

**(b) URINE** ..………………………………………………………………………….

**(c) CHEST** ……………………………………………………………………………….

**(d) BLOOD** ……………………………………………………………………….

**(e) EYES** ……………………………………………………………………………

**(f) EARS** ……………………………………………………………………………

**(g) HEART** ………………………………………………………………………..

**(h) STOMACH ULCERS** ……………………………………………………..

**(i) OTHERS**

……………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………

I am satisfied **/** not satisfied that the above named Student is physically and mentally fit to pursue further studies in Secondary School.

……………………………… ………………

**SIGNATURE (and official stamp)** **DATE**

……………………… ………………

**DESIGNATION**